TANGAZO LA SERIKALI Na. 50E la tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO ITOKANAYO NA HUDUMA YA USHAURI ELEKEZI WA KIHANDISI NA HUDUMA ZA UJENZI KATIKA MRADI WA UANZISHAJI WA KILIMO CHA MIWA NA UENDESHAJI WA MTAMBO WA KUZALISHA SUKARI WA KAMPUNI YA KAGERA SUGAR YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio Itokanayo na Huduma ya Ushauri Elekezi wa Kihandisi na Huduma za Ujenzi katika Mradi wa Uanzishaji wa Kilimo cha Miwa na Uendeshaji wa Mtambo wa Kuzalisha Sukari wa Kampuni ya Kagera Sugar ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 28 Juni, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya zuio inayopaswa kulipwa na Kampuni ya Kagera Sugar kwenye huduma za ushauri elekezi za kihandisi na huduma za ujenzi katika Mradi wa Uanzishaji wa Kilimo cha Miwa na Uendeshaji wa Mtambo wa Kuzalisha Sukari inasamehewa.

Ukomo

**3**. Amri hii itafikia ukomo wake tarehe 27 Juni, 2028 na inaweza kuongezewa muda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Kagera Sugar na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 25 Machi, 2022.

Dodoma,
31 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*